**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

# TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WABAJETI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

01 Aprili, 2026

**TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 62 na Ibara ya 63(2) na (3) imeainisha majukumu ya Ofisi ya Bunge ambayo ni kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge Sura 115 kama ilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2015, kilianzisha Mfuko wa Bunge, ili kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake na kinatoa maelekezo ya namna Mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele cha (c) cha Sheria ya Bajeti, Kamati ilikutana

na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula (Mb), Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Ndugu, Baraka I. Leonard - Katibu wa Bunge, ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Februari, 2026 pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/26.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura ya 410, Dira ya Taifa 2025, Mpango wa muda mrefu wa miaka 15, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26, Mpango wa Ofisi ya Bunge Mwaka 2021/22-2025/26 pamoja na Mwongozo wa Muda wa Kati wa Mwaka 2023/24 – 2025/26.

Aidha, utekelezaji wa bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika kulingana na mahitaji halisi kwa lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

### 2.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge ya Mwaka 2025/26 hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 186,753,635,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 25,632,628,000.00** ni Mishahara, **Shilingi 149,327,675,000.00** fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 11,793,332,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo, **Shilingi 11,385,882,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 407,450,000.00** ni fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa utekelezaji wa bajeti Ofisi ya Bunge ilipokea kwa njia ya uhamisho nje ya Fungu 42 jumla ya **Shilingi 4,429,340,865.75** kwa ajili ya kugharamia Mradi wa usimikaji wa mfumo wa sauti (Digital Congress Network – DCN) kwenye ukumbi wa Bunge na hivyo kufanya bajeti ya Ofisi ya Bunge kufika **Shilingi 191,182,975,865.75.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **Shilingi 113,923,024,121.18** zilipokelewa sawa na **asilimia 59.59** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya Fedha hizo, Mishahara ilikuwa **Shilingi 11,608,549,511,** Matumizi mengineyo **Shilingi 89,112,135,000** na matumizi ya maendeleo jumla ya **Shilingi 13,202,339,610.18** Aidha, kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi 12,868,039,610.18** ni fedha za ndani na **Shilingi 334,300,000.00** ni fedha za nje. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.1.**

**2.1.1 Jedwali Na. 1. Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge hadi Februari 2026**

| MAELEZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 25,632,628,000.00 | 11,608,549,511.00 | 45.29 |
| Matumizi Mengineyo | 149,327,675,000.00 | 89,112,135,000.00 | 59.68 |
| Maendeleo | 16,222,672,865.75 | 13,202,339,610.18 | 81.38 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **191,182,975,865.75** | **113,923,024,121.18** | **59.59** |

**Chanzo:** *Randama ya Mfuko wa Bunge*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kutoa fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya Mfuko wa Bunge ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

## 2.2 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya Maduhuli ya **Shilingi 147,966,000.00.** Hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **Shilingi 19,200,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 12.9** ya makisio yaliyopangwa. Fedha zilizokusanywa zimetokana na kodi ya pango katika Jengo la *Utawala Annex.* Mwenendo huo wa makusanyo ya maduhuli ulitokana na masharti ya kimkataba ambapo kodi ya pango hulipwa mwishoni mwa mwaka wa Fedha. Hivyo, mategemeo ni kukusanya **asilimia 100** ifikapo Juni, 2026.

## 2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026 Mfuko wa Bunge umefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu Mikutano ya Bunge, Vikao vya Kamati za Bunge, Ushiriki wa Mikutano ya Kimataifa pamoja na shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Ofisi ya Bunge. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Mikutano miwili (2) ya Bunge (Mkutano wa Kwanza - tarehe 11 hadi 14 Novemba 2025, Mkutano wa Pili - tarehe 27 Januari hadi 06 Februari 2026;
ii. Kufanya ununuzi wa Magari 6 kwa ajili ya kuhudumia Viongozi na Watumishi wa Bunge.
iii. Kuajiri watumishi wapya 28 kwenye kada mbalimbali ili kuongeza ufanisi na nguvu kazi;
iv. Kuratibu mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu uendeshaji wa Bunge na kamati zake;
v. Kuanda na kutekeleza Mpango Kazi wa Ununuzi wa Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26;
vi. Kusimika mfumo mpya wa Sauti *(Digital Congress Network* – DCN) katika ukumbi wa Bunge pamoja na kufanya marekebisho mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwajili ya kuongeza tija na ufanisi wa shughuli za Bunge;
vii. Kuboresha majengo ya ofisi pamoja na kumbi mbalimbali za mikutano kama vile ukumbi wa Msekwa na ukumbi Mkubwa wa Mkutano wa Bunge; na
viii. Kuandaa Hesabu ya Mwaka *(Annual Accounts)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na Taarifa za Ukaguzi kwa Mwaka wa fedha 2025/26.

## 2.4 Changamoto ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42). Ofisi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo ikiwemo: -

a) Kuwepo kwa shughuli ambazo hazikutengewa bajeti lakini ni muhimu kutekelezwa mathalani ongezeko la **Majimbo 8** ya Uchaguzi yaliyopelekea nyongeza ya Wabunge 11 hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji; na

b) Kupanda kwa mara kwa mara kwa gharama za bidhaa na huduma na kusababisha mahitaji ya uhamisho wa fedha ndani ya Fungu za matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizo, Ofisi ya Bunge imefanya mashauriano na Wizara ya Fedha kuhusu upatikanaji wa fedha ili kugharamia shughuli muhimu katika utendaji kazi wa Bunge na kuhakikisha ofisi inatekeleza shughuli zake kulingana na bajeti iliyotengwa na kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia utekelezaji wa bajeti. Hivyo, changamoto hizo hazitarajiwi kujitokeza Mwaka wa Fedha 2026/27.

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

**Mheshimiwa Spika,** makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 yamezingatia masuala yafuatayo:-

i. Dira ya Taifa (Dira 2050);
ii. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa muda mrefu wa miaka 25;
iii. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2026/2027 - 2030/203);
iv. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka mmoja wa mwaka mmoja (2026/2027);
v. Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge wa Mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031 unaotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja unaolenga kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza Majukumu yao ya Kikatiba kwa ufanisi;
vi. Majukumu ya Bunge Kikatiba;
vii. Malengo ya Taasisi;
viii. Majukumu ya Idara na vitengo;
ix. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
x. Sheria ya Bajeti Sura ya 439;
xi. Sheria ya Fedha za Umma Sura 348; na
xii. Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410.

## 3.1 Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/27 Mfuko wa Bunge umetengewa jumla wa **Shilingi 225,021,780,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 24,889,142,000.00** ni Mishahara, **Shilingi 183,103,656,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 17,028,982,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. kati ya kiasi kilichotengwa cha fedha za maendeleo, Shilingi **16,385,882,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 643,100,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti hiyo inatosheleza kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikatiba na kisheria.

## 3.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Mfuko wa Bunge umepanga kukusanya Maduhuli jumla ya **Shilingi 191,553,000.00** yatakayotokana na ukodishaji wa kumbi za mikutano Ofisi ndogo ya Bunge Dar es Salaam na kodi ya pango kwenye ya jengo la *Utawala Annex* pamoja na Mgahawa uliopo katika Jengo la Utawala Dodoma.

## 4.0 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA 2026/27

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kugharamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Bunge;
ii. Kugharamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Bunge;
iii. Kugharamia Posho ya Jimbo, Usafiri na Stahili nyingine kwa Wabunge na Watumishi;
iv. Kugharamia Matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi pamoja na Watumishi;
v. Kuboresha maslahi ya Wabunge na Watumishi;
vi. Kugharamia mafunzo kwa Wabunge na Watumishi;
vii. Kuhudumia Viongozi Wastaafu wa Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya kustaafu ya Viongozi wa Kisiasa;
viii. Ununuzi wa Samani za Ofisi kwa ajili ya Viongozi na Watumishi;
ix. Ununuzi wa Vitendea Kazi *(Computer, Laptop/Ipad, Printer, Photocopier and Shredder)* kwa Watumishi;
x. Ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa, hususan mikutano ya Vyama vya Kibunge ambavyo Bunge letu ni Mwanachama;
xi. Kuwa mwenyeji wa mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

xii. Kushiriki katika michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki na Shimiwi;

xiii. Kugharamia maadhimisho ya sherehe ya Kutimiza Miaka 100 ya Bunge la Tanzania;

xiv. Kugharamia uanzishwaji wa Taasisi ya Mafunzo ya Kibunge;

xv. Maboresho ya Mifumo ya TEHAMA ukiwemo Mfumo wa Bunge Mtandao *(e-parliament);*

xvi. Marekebisho ya Miundombinu ya TEHAMA katika Majengo ya Ofisi;

xvii. Kugharamia urushaji wa matangazo ya Bunge Mbashara kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pamoja na mikutano ya Elimu kwa Umma;

xviii. Kugharamia gharama nyingine za uendeshaji wa Ofisi zikiwemo umeme, maji, usafiri, usafi na ulinzi;

xix. Kufanya Ukarabati Ofisi ya Dar es Salaam na Nyumba za Viongozi;

xx. Kuendelea kuboresha Mfumo wa Sauti (DCN) katika Ukumbi wa Bunge;

xxi. Kusimika Mitambo ya Usalama katika maeneo ya majengo ya Ofisi; na

xxii. Ujenzi wa Uzio kuzunguka eneo la Bunge.

## 5.0 MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni yafuatayo:-

### 5.1 Uendelezaji wa Maeneo Mapya ya Ofisi za Bunge Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa awamu ili kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili wzitumie kwenye viunga vya Bunge. Hatua hii itasaidia kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi zao za kiofisi ndani ya viunga vya Bunge, sehemu ambayo itakuwa salama na inazingatia usiri.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kutoa pole kwa Familia, Wabunge wote na Serikali kwa kuondokewa na Mhe. William Lukuvi (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, ***Hakika Bunge limepoteza Muwakilishi hodari, mahiri, mchapakazi na mzalendo.***

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) Spika wa Bunge pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb) Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Bal. Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Mshamu Ali Munde, (Mb), Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ally Hassan Omar King, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bal.Dkt. Pindi Azara Chana, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Enock Zadock Koola, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye j umla ya **Shilingi 225,021,780,000** ambapo kiasi cha **Shilingi 24,889,142,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 183,103,656,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 17,028,982,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

01 Aprili, 2026